*[OKTOBA, 2024]*

**BUNGE LA KUMI NA TATU – KIPINDI CHA TATU (2024)**
**BUNGE LA TAIFA**

# KWA MUJIBU WA USHUGHULIKIAJI WA HOJA MAALUM YA KUONDOLEWA OFISINI KUPITIA MASHTAKA KWA NAIBU RAIS WA JAMHURI YA KENYA

## FOMU YA MAONI YA UMMA

*(Kwa mujibu wa Ibara 1(2), 10(2)(A) na 118 za Katiba)*

---

**Sehemu ya A: Taarifa za Kibinafsi**

1. Jina: ____________________________________________
2. Jinsia: __________________
3. Eneobunge____________________________________________
4. Kaunti____________________________________________
5. Nambari ya *(Kitambulisho/Pasipoti/Leseni ya Udereva ya Kenya)*________________

**Sehemu ya B: Maoni kuhusu pendekezo la Hoja Maalum ya kumwondoa ofisini Naibu Rais**

6. Je, maoni yako kuhusu Hoja hii ni yapi? (*Weka alama*)

☐ Ninaunga mkono

☐ Ninapinga.

☐ Mengine (Eleza) ____________________________________________

____________________________________________

7. Ikiwa unaunga mkono, taja msingi au misingi unayokubaliana nayo kwenye Hoja Maalum kama ilivyofupishwa hapa chini. *(Weka alama kwa misingi unayokubaliana nayo)*—

☐ **Ukiukaji Mkubwa wa Ibara 10(2)(a), (b) na (c); 27(4), 73(1)(a) na (2)(b); 75(1)(c), 129(2) na 147(1) za Katiba, zikisomwa na Ibara 131(2)(c) na 131(2)(d) za Katiba.** Hoja Maalum inadai kwamba Mhe. Naibu Rais amekuwa akitoa kauli zinazotisha kubagua, kutenga na kinyume cha sheria kunyima baadhi ya Wakenya na maeneo ya Jamhuri ya Kenya fursa sawa kupitia teuzi za huduma kwa umma na ugavi wa rasilimali za umma.

☐ **Ukiukaji Mkubwa wa Ibara 147(1) na 152(1) za Katiba kwa kuhujumu Rais, Baraza la Mawaziri, na utekelezaji mzuri wa mamlaka kuu ya serikali kuu ya taifa.** Hoja Maalum inadai kwamba Mhe. Naibu Rais ametoa kauli za kupendelea upande mmoja hadharani, kauli zinazopingana na misimamo ya kisera iliyopitishwa na Serikali, na kukinzana na Rais kuhusu masuala muhimu ya utawala na utekelezaji wa kazi ya Rais kama ishara ya umoja wa taifa.

☐ **Ukiukaji Mkubwa wa Ibara 6(2), 10(2)(a), 174, 186(1), 189(1) na Nyongeza ya Nne ya Katiba kwa kuhujumu Ugatuzi.** Hoja Maalum inadai kwamba Mhe. Naibu Rais aliingilia uendeshaji wa Serikali ya Kaunti ya Jiji la Nairobi kwa kuchochea wananchi dhidi ya maagizo halali ya Serikali ya Kaunti kuhusu upangaji na uhamishaji wa masoko na akadhalilisha hadharani uongozi wa Serikali ya Kaunti na maamuzi yake.

☐ **Ukiukaji Mkubwa wa Ibara ya 160(1) ya Katiba kuhusu Uhuru wa Kiasasi na Uamuzi wa Majaji.** Hoja Maalum inadai kwamba Mhe. Naibu Rais amehujumu uhuru wa kiasasi na kimaamuzi wa majaji kwa kumshambulia hadharani jaji wa Mahakama Kuu ya Kenya na kutoa vitisho vya uongo kwamba atawasilisha ardhilhali ya kumwondoa jaji huyo katika kesi inayomhusu Naibu wa Rais.

☐ **Ukiukaji Mkubwa wa Ibara 3(1) na148(5)(a) ya Katiba kuhusu Uaminifu kwa Kiapo cha Uadilifu na Utiifu.** Hoja Maalum inadai kwamba Mhe. Naibu Rais alivunja Kiapo chake cha Uadilifu na Utiifu kupitia matamshi na matendo yanayohusishwa na Naibu Rais kulingana na Misingi (1), (2), na (3) ya Hoja Maalum**.**

☐ **Sababu za dhati za kuamini kwamba Mhe. Naibu Rais ametenda makosa ya jinai kwa mujibu wa vifungu 13 (1) (a) na 62 vya Sheria ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa.** Hoja Maalum inadai kwamba Mhe. Naibu Rais amekuwa akitoa matamshi ya kuhamakisha, yasiyo na uwajibikaji, na ya uchochezi hadharani katika miaka miwili iliyopita kinyume na sheria.

☐ **Sababu za dhati za kuamini kuwa Mhe. Naibu Rais ametenda makosa makubwa ya jinai ya kiuchumi kwa mujibu wa vifungu 45(1), 46, 47(a) (3), na 48(1) vya Sheria ya Kupambana na Ufisadi na Uhalifu wa Kiuchumi na vifungu vya 2, 3, 4, na 7 vya Sheria ya Mapato ya Uhalifu na Kupambana na Utakatishaji wa Pesa.** Hoja Maalum inadai kwamba Mhe. Naibu Rais ametenda makosa makubwa ya jinai ya kiuchumi ambayo ni mkinzano wa kimasilahi, matumizi mabaya ya mamlaka, kupanga njama ya kutenda makosa ya jinai kwa kujilimbikizia mali yenye thamani ya takriban shilingi bilioni 5.2 za Kenya kwa njia zisizoelezeka na ambayo hailingani na mapato yake halali yanayojulikana, na kwa kufanya biashara na Ofisi ya Naibu Rais kupitia kwa mawakala.

☐ **Sababu ya dhati ya kuamini kwamba Mhe. Naibu Rais ametenda makosa ya jinai kwa kuendelea kupotosha umma kupitia matamshi ya uongo, yenye nia mbaya, yanayoleta utengano na uchochezi kinyume na masharti ya kifungu cha 132 cha Kanuni ya Adhabu na kifungu cha 29 cha Sheria ya Uongozi na Uadilifu.**

☐ **Utovu Mkubwa wa Nidhamu unaokinzana na hadhi ya Ofisi ya Naibu Rais, mjumbe wa Baraza la Mawaziri, na mjumbe wa Baraza la Usalama la Taifa.** Hoja Maalum inadai kwamba Mhe. Naibu Rais ameshambulia hadharani na kuhujumu kazi ya Huduma ya Usalama wa Taifa na Ujasusi, na maafisa wake.

☐ **Utovu Mkubwa wa Nidhamu kwa kumkaidi Rais, ambaye ni Kiongozi wa Taifa na Serikali, wazi na hadharani.**

☐ **Utovu Mkubwa wa Nidhamu kwa kuendelea kusuta maafisa wa serikali na wa umma.** Hoja Maalum inadai kwamba Mhe. Naibu Rais, kwa miaka miwili iliyopita, amekuwa akiwasuta maafisa wa serikali na umma.

**SAINI _______________TAREHE: ______Oktoba 2024**

**Maagizo:**

*__Pakua__ fomu hii kutoka kwa www.parliament.go.ke na **uijaze**. Fomu iliyojazwa inaweza kuwasilishwa katika kituo au sehemu ya kupokea maoni ilivyoorodheshwa katika mpangilio wa vikao vya kupokea maoni ya umma Ijumaa, **tarehe 4 Oktoba 2024,** au kutumwa kwa Katibu wa Bunge la Taifa, S.L.P. 41842-00100, Nairobi, au kuwasilishwa kwa Ofisi ya Katibu wa Bunge la Taifa katika Majengo Makuu ya Bunge, Nairobi, au kutuma baruapepe kupitia anwani impeachment@parliament.go.ke ili ipokewe kabla au Jumamosi **tarehe 5 Oktoba 2024** saa kumi na moja jioni.

*Shukrani: Bunge la Taifa linakushukuru kwa kushiriki katika zoezi hili.*